

UTARATIBU WA UMILIKISHA WA ARDHI (SUB-TITTLE) KWA MWEKEZAJI WA KAMPUNI YA CRJE (EAST AFRICA) LIMITED

1.0 UTANGULIZI

Utaratibu wa umilikishaji ardhi kwa wawekezaji wenye Sub-Tittle ni mpya na umewahi kufanyika mara moja kwa mwekezaji wa Kampuni ya Cedex Investment Limited baada ya majadiliano ya muda mrefu na Kamishna wa Ardhi juu ya utaratibu utakatumika kumilikisha Ardhi hiyo na mwekezaji kupewa Hatimiliki isiyo ya asili (*Derivative Rights*).

2.0 UTARATIBU UTAKAOTUMIKA

Kutokana na maelekezo ya Kamishna yaliyopelekea kukamilisha utaratibu wa umilikishaji wa ardhi na kutoa Derivative Right kwa Cedex Investment Limited. Mwekezaji huyu pia atazingatia utaratibu ufuatao;

- i. Mwekezaji na Muuzaji wa eneo lenye Sub-Tittle atasaini mkataba wa mauziano kama inavyofanyika kwenye viwanja vya kawaida;
- ii. Mwekezaji/ Muuzaji watalipa kodi zote za serikali kwa mujibu wa sheria;
- iii. Baada ya kukamilisha taratibu za hapo juu TIC itaandaa nyaraka inayoitwa *Transmission by Operation of Law* nyaraka hiyo itasainiwa na Mtendaji Mkuu kisha itawasilishwa kwa Msajili wa Hati Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam ikiwa na mikataba ya mauziano na Sub-Tittles za eneo husika. Msajili wa hati Msaidizi atasajili Sub-Tittles hizo kwa jina la TIC;
- iv. Fomu ya Ardhi Na. 1 itasainiwa na eneo hilo litatangazwa kuwa la Uwekezaji;
- v. Eneo husika litapelekwa kwenye Kamati ya Taifa ya kugawa ardhi kwa ajili ya kupitisha
- vi. Mwekezaji anaandaliwa Hatimiliki isiyo ya asili (*Derivative Right*) na TIC. Aidha, DR itakayoandaliwa kwa utaratibu huu itakuwa na **muda wa umiliki uliopo kwenye Sub-Tittle kwa mujibu wa Hati iliyowasilishwa muda uliobaaki ni miaka 70 kwani miliki imeanza tarehe 1.04. 1999** sio kuanza muda wa umiliki upya wa miaka 99 na kisha mwekezaji atapewa *Derivative Right*. Utaratibu wa kurejesha milki (surrender) na kutoa milki ya miaka 99 kwa TIC hauwezi kutumika kwenye Sub-Tittle kwa sababu ukirejesha milki ya sehemu ya jengo utaathiri jengo zima ambalo wamiliki wake ni tofauti.

3.0 HITIMISHO

Mwekezaji wa Kampuni ya CRJE (East Africa) Limited amejulishwa juu ya utaratibu huu kupitia mwasheria wake wa Kampuni ya Aymak Attorney Bw. Peter Kanya mwenye namba ya simu **Na. +255 718 000426** ambaye amekuwa akifatilia kusajili mradi huu TIC. Amekiri kuelewa utaratibu huu na kuomba TIC iendelee na usajili wa mradi.